# LEARNING BY EAR 2012

## “Bado ningali mwanadamu – Riwaya inayoangazia matatizo wanayopata wauguaji wa maradhi ya akili barani Afrika”

## EPISODE 7: “Chimbuko la itikadi"

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**

**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: MALEMBA NA CHUMBA WANAMTEMBELEA DKT. MAHIRO**

- **Malemba (MKE, 35)**
- **Mahiro ( MUME, 50)´**
- **MSIMULIZI**

**SCENE TWO: VALERIE AMFUATA IRENE CHUONI**

- **Valerie (MKE, 19)**
- **Irene (MKE, 19)**
- **MSIMULIZI**

**SCENE THREE: KAPAKA ZIARA YA DKT. MAHIRO**

- **Kapaka (MUME, 25)**
- **Mahiro (MUME, 50)**

**UTANGULIZI:**

Nakusabahi nikikualika tena katika **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Hadithi yetu inaitwa, **“Bado ningali mwanadamu”.** Ambayo inaangazia wale wanaogua maradhi ya akili barani Afrika. Katika vipindi vilivyopita tumejionea jinsi ilivyokuwa vigumu kwa watu kuyakubali maradhi haya ya akili kama maradhi mengine. Lakini kupuuza huku, kutowajibika, na kukosa huruma kwa wagonjwa hawa wa akili kunatokana na nini? Ndiyo tuko karibu kujua katika kipindi hiki cha leo kwa jina “ **Chimbuko la itikadi”** tunaanza na Malemba na kijana wake Chumba wakimsubiri Dkt. Mahiro jijini. Walidamka asubuhi na mapema na kuwa wa kwanza kwenye mstari mlangoni.

**SCENE ONE: MALEMBA NA CHUMBA WAMTEMBELEA DAKTARI MAHIRO**

1. **ATMO: HOSPITAL AMBIENCE (INSIDE DOCTOR’S ROOM)**
2. **MAHIRO:** **(calls out)** Mwengine!
3. **MALEMBA:** Habari ya asubuhi.
4. **MAHIRO:** Njema, niwasaidie na nini?
5. **MALEMBA:** Ni kijana wangu. Anaitwa Chumba. Sijui

nikuelezeje. Ninavyoona mimi ni kuwa amepagawa na pepo, lakini la kushangaza ni kwanini wamfanye yeye ndiye kiti. Nimemleta kwako kwa minajili ya kumpa msaada, ili na mimi nipumzike. Kwa sababu nimejaribu njia zote lakini sikufaulu.

6. **MAHIRO:** Mmh … sawa, haswa tatizo lake nini? Kipi kinachokufanya uone hana akili timamu?

7. **MALEMBA:** Kwanza, ana miaka 16 sasa, lakini bado maongezi yake ni ya thathathatha... na hapo vikimdidimka ndiyo husema na asieleweke anasema nini kabisa, haswa anapoudhiwa au kukasirishwa. Hufanya hivyo akijirudia mara kwa mara, na unavyomuona ni yeye peke yake, mpweke hana rafiki wala sahiba. Yuko kando kando saa zote, yuko kwenye ulimwengu wake na hataki maoni ya mtu.

8. **MAHIRO:** Alianza hali hiyo lini? Unaweza kukumbuka alianza kuonyesha ishara hizo lini?

9. **MALEMBA:** Nilianza kumshuku kuwa hayuko sawa alipotimiza umri wa mwaka moja na nusu. Alizaliwa sawa, kama mtoto mwingine halafu ndio akaanza tatizo la kusahau chochote anachofunzwa shuleni au hata nyumbani, akaanza kujitenga na marika zake akawa hachezi, kutamka maneno ni shida na

kadhalika. Nilifikiri akikuwa ataacha arudie hali yake ya kawaida, ikawa sivyo. Kwa miaka 14, nimevumilia uchungu wa kumuona mwanangu akikua kijana mkubwa katika hali hii.

10. **MAHIRO:** Kwa hivyo, kulingana na maneno yako, inaonekana kijana wako ni kirunda. Anaugua maradhi ambayo katika ulingo wa matibabu kitaalamu yanajulikana kama “regressive autism”. Hii ni hali inayomtokea mtoto kabla au afikapo miaka mitatu, na huathiri ukuaji wa akili katika mambo ya kutangamana na kujieleza. Ni hali tatanishi hasa kwa Afrika ambapo wengi hawana ufahamu nayo.

11. **MALEMBA:** Urundifu, umesema hivyo. Sawa daktari, unatibika kweli?

12. **MAHIRO:** Kwanini usitibike panapo matibabu, nyingi za ishara zake hutibika, ijapo athari yake wengine hubakia nayo maisha. Lakini hilo haliwazuii waathiriwa hao kuishi na familia au watu wao.

13. **MALEMBA:** Kumaanisha kuwa Chumba ataishi hivi maisha yake yote?

14. **MAHIRO:** Nimesema panapo mazoezi na matibabu hali hii hutibika, lakini athari yake haitoisha kabisa. Lazima tumfanyie utafiti mwengine ndiyo tuwe na

uhakika. Utafiti mwingi hata hivyo, unazidi kufanyiwa kuhusiana na maradhi haya. Muhimu ni kujua kuwa Chumba siye anayeugua maradhi haya peke yake. Wapo vijana na watoto wengi wenye shida kama hii. Wavulana huathirika mara nne zaidi kuliko wasichana. Ijapo hamna takwimu za kuaminika kuhusu wale walioathirika na ugonjwa huu, lakini makadirio ni kuwa kati ya watu elfu moja, kuna mtu mmoja au wawili anayeugua maradhi haya. Na wanazidi kuongezeka.

15. **MALEMBA:** Hmm… na husababishwa na nini? Ni uchawi kama vile majirani zangu wanavyoamini? Au ni majini kama niaminivyo mimi? Huletwa na nini haswa, daktari?

16. **MAHIRO:** Maradhi ya “autism” hayana chanzo maalum. Wataalamu wameshuku mengi, lakini hakuna jawabu sahihi. Wengine hufikiri husababishwa na madini ya “mercury”, yaani –zebaki- au kuzaa watoto ukiwa na umri mkubwa. Wengi wanasema ugonjwa huu waweza kuurithi au pia kuletwa na hali ya mazingira. Lakini ukweli ni kuwa hakuna chanzo maalum.

17. **MALEMBA:** Basi ni kweli ni laana. Mmoja katika familia yetu lazima alitenda uovu ambao kulipwa kwake kunanitesea mtoto wangu namna hii.

**18. MAHIRO:** Mama, mimi ni mtaalamu wa akili na kazi yangu ni kukueleza mtoto wako ana shida gani. Siwezi kukuaminisha zaidi kama huamini hayo ninayokueleza.
Njoo tena kesho na mtoto wako. Nitamfanyia utafiti mwengine kuhusiana na hali yake hiyo, pia tuanze matibabu yake. Ijapokuwa tayari ana miaka 16, basi matibabu yanaweza kufaulu au kutofaulu.

**19. MALEMBA:** Asante daktari. Nashukuru kwa kukubali kutumia muda wako mwingi na najua wengi wanasubiria huko nje.

**20. MAHIRO:** Hamna wasiwasi. Kuhusu huo mlolongo huko nje: unazidi kuwa mrefu na mrefu kila kukicha, wakati rasilimali za kukabiliana na maradhi ya akili zinazidi kupungua. Uwe na siku njema.

**21. MSIMULIZI:** Utafiti mchache sana umethibitishiwa maradhi ya urunda barani Afrika. Lakini ukweli ni kuwa: maradhi ya akili yanaathiri wengi. Ijapokuwa familia nyingi zinakumbana na matatizo haya, jamii, majirani na wengineo hawana habari kuhusu maradhi haya, hivyo kuacha mila na desturi zao kuwapa sababu yake. Dakika hizo chache tu, Malemba ametolewa taka masikioni. Anampeleka Chumba nyumbani kwa kakake. Wanapotoka kwa chumba cha utafiti cha Dokta Mahiro, mvua ilianza kunyesha huko nje. Kwenye jiji hilo hilo, Valerie amesimama nje ya chumba cha sahiba wake Irene, amelowa

chapachapa kwa mvua, hajala na amepigwa na baridi usiku mzima. Koti alilopewa na Irene limelowana, na mkononi mwake, ameshika kipande cha mkate alichookota jalalani.

**SCENE TWO: VALERIE RETURNS TO IRENE AT THE COLLEGE**

22. **ATMO:** **HEAVY RAIN AND THUNDERSTORM OUTSIDE (HEARD FROM INSIDE)**

23. **VALERIE:** **(calling out)** Irene... Irene… nifungulie!

24. **SFX:** **KNOCKING ON DOOR**

25. **IRENE:** **(from inside)** Ni nani? Kuna nini mapema hivi. Sawa, subiri, naja kufungua.

26. **SFX:** **DOOR BEING UNLOCKED AND OPENED**

27. **VALERIE:** Nimekuletea koti lako, Irene.

28. **IRENE:** **(pleasant surprise)** Valerie! Lo ni vyema nimekuona. Ulinishtusha ulipopotea jana kule mitaani. Alafu ukanitoroka… sikujua una mbio namna ile. Lakini karibu… hebu ingia ndani kabla watu hawajakuona ukiwa namna hii.

29. **SFX:** **DOOR BEING CLOSED**

**30. VALERIE:** Narudi. Sikupanga kukawia.

**31. IRENE:** Valerie… ni sawa. Huhitaji kuogopa. Uko salama na ukiwa na mimi, usiwe na wasiwasi, nakuhakikishia hilo.

**32. VALERIE:** Hakuna aliye salama. Hata wewe. **(starts to cry)** Nahisi baridi, nimechoka… naogopa.

**33. IRENE:** Sababu unatembea mwendo mrefu bila nguo, kun nyesha na uko na nguo mbichi mwilini, Valerie. Na nani kakupa kipande hicho cha mkate? Hebu ingia ndani uoge huku nikikuandalia stafstahi. Sawa?

**34. VALERIE:** Sawa.

**35. IRENE:** Vyema. Haya kaoge basi, nakuandalia kifungua kinywa kwanza, halafu nikuletee nguo. Natumai zitakutosha. Umekonda sana! Na kisha, Valerie, baadae tutakwenda kumtebelea rafiki yangu. Najua mmeshawahi kukutana nae kitambo. Lakini kwanza tuanze na kuoga halafu chai.

**36. VALERIE:** Sawa... ni sawa. Asante. Asante sana.

**37. MSIMULIZI:** Irene anafurahi kumuona Valerie. Baada ya kumkimbiza usiku kucha bila kumkamata, alikata tamaa ya kumuona tena. Lakini Valerie huyu hapa, tena kajileta mwenyewe. Wakati Irene

anatayarisha kiamsha kinywa, Valerie akikubaliana na kila kitu alichoambiwa na Irene, Dkt. Mahiro alikuwa akimuona mteja mwengine wa umri wa miaka 20 hivi. Endelea kutega sikio.

**SCENE THREE: KAPAKA AMTEMBELEA DKT. MAHIRO**

38. **ATMO:** **DR. MAHIRO’S ROOM**

39. **MAHIRO:** **(calls out)** Mwengine tafadhali!

40. **SFX:** **CREAKING SOUND WHEN DOOR OPENED**

41. **MAHIRO:** Naam, kijana. Nikupe msaada gani?

42. **KAPAKA:** Jina langu ni Kapaka. Naamini kuwa nimekuja hapa baada ya jaribio la kujitoa roho.

43. **MAHIRO:** Sawa, Kapaka, hebu nifungie huo mlango? Tunahitaji kuzungumza tukiwa faragha.

44. **SFX:** **DOOR CLOSED**

45. **MAHIRO:** Umeniambia, karibu ujiue. Unaweza kuniambia ni kwanini?

46. **KAPAKA:** Nilianza kuwa na mawazo hayo baada ya kuachishwa kazi. Bosi alikuwa na madai kuwa nimemuibia pesa zake, naweza kuapa hata leo kuwa sikuwahi. Nilijaribu kumueleza lakini

akanipuuza.

47. **MAHIRO:** Na hili tukio lilitokea lini?

48. **KAPAKA:** Kama miezi miwili iliyopita. Mke wangu alikuwa na mimba ya mtoto wetu wa kwanza. Alijifungua hivi majuzi binti yetu.

49. **MAHIRO:** Ah, nakupa hongera, kwa hivyo wewe sasa unaitwa babake mtu...

50. **KAPAKA:** Ndio, lakini baba asiye na maana, wenyewe humuita baba sukari ya mraba. Sioni hata maana ya haya maisha. Sijawahi kuhisi hivi. Kila kitu kimekosa maana kwangu.

51. **MAHIRO:** Sawa, Kapaka, unapendelea kufanya nini wakati hauko kazini?

52. **KAPAKA:** Nilipendelea kuimba kwaya kanisani. Lakini sasa hiyo hamu sina tena. Tangu nipoteze kazi yangu hupenda kukaa ndani peke yangu, niliwahi kutoka nje mara mbili tu, wakati mke wangu alipojifungua na wakati mchungaji aliponishauri twende kwa matembezi...

53. **MAHIRO:** Nafurahi, Kapaka, ulikubali ushauri huo. Bila shaka unaugua maradhi ambayo wataalamu wanaita “severe depression”, ni vyema kuwa

hukujitoa uhai. “Depression” ni hali ambayo inaweza kutibiwa na ukaendelea na maisha yako kama kawaida. Bora ukubali kutumia matibabu na ujipe moyo mpaka utakapotibika.

54. **KAPAKA:** Na je kuhusu kazi? Nitaajiriwa tena kweli?

55. **MAHIRO:** Sioni sababu ya kutoajiriwa. Bali kwanza ni muhimu ujiweke sawa kiakili. Kisha utafute kazi. Nieleze, Kapaka, saa hizi unahisi vipi? Akili yako inakutuma nini?

56. **KAPAKA:** Kwa sasa nimechanganyikiwa. Naona kuja hapa ni kama nimefanya vizuri, halafu pia naona kama napoteza wakati.

57. **MAHIRO:** Vyema. Kwamba unajifikiria hali yako, tayari ni dalili njema. Nataka tuonane kwa juma mara moja. Na nitakuandikia dawa. Kisha nakushauri usikae mpweke jishughulishe na mambo unayopenda kufanya. Kama hutaki kuimba basi tafuta jengine. Kama kucheza na binti yako au kufanya matembezi na familia yako. Nakutakia uponyaji wa haraka Kapaka, nasisitiza tena kuwa umefanya uamuzi wa busara kunitembelea.

**HITIMISHO:**

Basi hapo tunahitimisha kipindi hiki cha saba cha hadithi yetu ya maradhi ya akili barani Afrika. Jiunge nasi kipindi kijacho tukupashe

kuhusu masaibu ya kina Kapaka na wengineo. Uhitajipo kusikiliza tena kipindi hiki au kingine kilichopita tembelea tovuti yetu www.dw.de/lbe. Mpaka tutakapokutana tena, kwaheri na ubaki salama.